

هذه عقیدتي

Hii ndio 'Aqiydah yangu


Mwandishi

Imaam 'Abdul-'Aziyz bin 'Abdillaah bin Baaz

Tarjama:

www.wanachuoni.com

Swali:.....	3
2. Allaah yuko juu ya viumbe wote na amelingana juu ya 'Arshi	4
3. Ni wajibu kuamini na kuthibitisha majina na sifa za Allaah	5
4. Majina na sifa za Allaah ni Tawqiyfiiyah.....	5
5. Qur-aan ni maneno ya Allaah	6
6. Kuamini yale yote yaliyoelezwa na Allaah na Mtume Wake	6



as-Salaam 'alaykum wa Rahmatullaahi wa Barakaatuh

Swali: Ni ipi 'Aqiydah yako ambayo unamuabudu Allaah kwayo kuhusu majina na sifa Zake na khaswa inapokuja katika kuthibitisha sifa ya Ujuu kwa Mola wetu (Tabaarak wa Ta'ala). Nataraji jibu kwa kifupi Allaah akubariki na elimu yako.

2. Allaah yuko juu ya viumbe wote na amelingana juu ya 'Arshi

Jibu: Wa 'alaykumus-Salaam wa Rahmatullaahi wa Barakaatuh

'Aqiydah ambayo ninamuabudu Allaah kwayo na ninamuomba Allaah (Subhaanah) anifishe juu yake ni:

Kuamini kuwa Yeye (Subhaanah) ndiye Mola wa haki ambaye anastahiki 'ibaadah na kwamba Yeye (Subhaanah) yuko juu ya 'Arshi na amelingana juu yake kulingana ambako kunalingana na Utukufu na Ukubwa Wake bila ya kumfanyia namna. Hakika Yeye (Subhanaah) anasifika kuwa juu ya viumbe wote. Amesema (Subhaanah):

الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى

"Mwingi wa Rahmah amelingana juu ya 'Arshi."¹

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ

"Hakika Mola wenu ni Allaah Ambaye Ameumba mbingu na ardhi katika siku sita halafu akalingana juu ya 'Arshi."²

وَلَا يَنْهَا دُهْنُهُمَا ۝ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ

"Wala hakumchoshi kuvihifadhi viwili hivyo. Naye yuko juu na ametukuka."³

فَالْحُكْمُ لِلَّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ

"Basi [leo] hukumu ni ya Allaah Pekee; Aliye juu na Mkubwa."⁴

إِنَّهُ يَصْنَعُ الْكَلِمَ الطَّيِّبَ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ

"Kwake Yeye linapanda neno zuri na kitendo chema hukinyanya."⁵

¹ 20:05

² 07:54

³ 02:2255

⁴ 40:12

⁵ 35:10

Aayah zilizo na maana kama hii ni nyingi.

3. Ni wajibu kuamini na kuthibitisha majina na sifa za Allaah

Ninaamini kuwa Yeye (Subhaanah) ana majina mazuri na sifa kuu. Amesema ('Azza wa Jall):

وَلِلّٰهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا

"Na Allaah Ana Majina Mazuri kabisa, basi muombeni kwayo."⁶

Lililo la wajibu kwa waislamu wote ni kuamini majina na sifa Zake zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah na kumthibitishia nazo kwa njia inayolingana na Utukufu Wake pasi na kuzipotosha, kuzikanusha, kuzifanyia namna na kuzilinganisha. Iwe kama alivyosema (Subhaanah):

لَيْسَ كَوْثِيلٌ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona."⁷

فَلَا تَضْرِبُو لِلّٰهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

"Basi msimpigie mifano Allaah, kwani Hakika Allaah Anajua nanyi hamjui."⁸

قُلْ هُوَ اللّٰهُ أَحَدٌ اللّٰهُ الصَّمَدُ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَّهُ كُفُواً أَحَدٌ

"Sema: "Yeye ni Allaahu Mmoja Pekee. Allaah ni Mwenye kukusudiwa. Hakuzaa na wala Hakuzaliwa. Na wala haiwi Awe na ye yote anayefanana [au kulingana] Naye."⁹

4. Majina na sifa za Allaah ni Tawqiyfiyyah

Majina na sifa za Allaah ni kukomeka (Tawqiyfiyyah). Ikiwa na maana ya kwamba haijuzu kuthibitisha chochote katika hayo isipokuwa kwa kuwepo dalili ima ya Qur-aan au Sunnah Swahiyh. Yeye (Subhaanah) ndiye anajijua

⁶ 07:180

⁷ 42:11

⁸ 61:74

⁹ 112:01-04

Mwenyewe na kujua yale yanayomstahikia. Vilevile Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) ndiye mwenye kumjua zaidi na ndiye mwenye kufikisha kutoka Kwake. Isitoshe jengine ni kuwa hazungumzi kwa matamanio yake. Amesema (Subhaanah):

وَالنَّجْمٌ إِذَا هَوَىٰ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا عَوَىٰ وَمَا يَطْقُنُ عَنِ الْهُوَىٰ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ

"Naapa kwa nyota inapotua. Hakupotea sahibu yenu na wala hakukosea. Na wala hatamki kwa matamanio. Hayo [ayasemayo] si chochote isipokuwa ni Wahy unaofunuliwa [kwake]."¹⁰

5. Qur-aan ni maneno ya Allaah

Ninaamini kuwa Qur-aan ni maneno ya Allaah ('Azza wa Jall) na hayakuumbwa. Hivi ndivyo wasemavyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa'ah katika Maswahabah wa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) na waliokuja baada yake.

6. Kuamini yale yote yaliyoelezwa na Allaah na Mtume Wake

Ninaamini yale yote aliyoelezea Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam) katika maelezo kuhusu Pepo na Moto, hesabu na malipo na yasiyokuwa hayo katika mambo yaliyowahi kuwepo na yatayokuwepo. Aidha yawe yametolewa dalili na Qur-aan au Sunnah Swahiyih kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa sallam).

as-Salaam 'alaykum wa Rahmatullaahi wa Barakaatuh

¹⁰ 53:01-04